[D591]

# Mwanamke wa Ufunuo 12

Ufunuo 12:1 KJV  Na ishara kuu ilionekana mbinguni;mwanamke aliyevikwa jua,na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake,na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili:

*Jua* kama ishara inaonyesha nuru ya Injili,yaani ukweli-ambao ni Kristo Yesu. *Mwezi* kama ishara unaonyesha nuru ya Sheria ya Musa. Mwezi ni akisi ya jua,kwa hivyo Sheria ilikuwa kivuli au onyesho lililokuwa kabla ya Injili. Nyota kama ishara zaonyesha walimu wa kanisa waliotiwa msukumo-yaani mitume. *Mbingu* kama ilivyoonyeshwa zinawakilisha nguvu za kanisa ya Ukristo. Mchanganyiko wa ishara hizi unapatikana katika *Ufunuo (12:1*) ambapo "mwanamke" ambaye anasimamia Kanisa la awali anaonyeshwa akivaa jua,yaani ameng'aa sana,na mwanga wa Habari Njema. *Mwezi* uliokuwa chini ya miguu yake unasimamia Sheria ambayo inamsaidia lakini sio chanzo cha nuru yake. Nyota kumi na mbili zinazopatikana juu ya kichwa chake kama taji zinaonyesha walimu wake walioteuliwa na kutiwa msukumo-yaani mitume kumi na wawili.

Na kwa kutoa muhtasari wa maana ya ishara hizi katika mawazo yetu, basi twaweza kuangalia kwa kina kipengele cha unabii mkubwa wa Bwana wetu wa ishara ambazo zinaonyesha mwisho wa ulimwengu huu.

Wakati wowote tukiangalia twagundua hakika kwamba wakati watu wa Mungu waliowekwa wakfu wanalishwa na kupewa mwanga kwa wakati huu, lakini Wakristo wa kawaida hawalishwi na hawana mwanga. Kiini cha mwanga wa Injili kuanzia mwanzo ni *msalaba* wa Kristo, yaani fidia; hata hivyo Papa alianzisha dhabihu ya ushindani ya Misa, watakatifu wa Mungu mara nyingi wameshindania ahadi zote za Mungu na matumaini yote aliyowapa wanadamu. Wameishika hata kama filosofia yake imefichika katika mitazamo yao.

Ukweli kuna wachache  ambao kwa kukosa kuelewa fidia, na kushindwa kuunganisha na kweli nyingine, na hasa kwa makosa yao,wameipuuza. Hawa hata hivyo ni watu adimu sana kwa sheria- kikwazo hapa kimeleta mafanikio,mpaka leo wanaokiri kuwa wahudumu wa msalaba *wanagundua* thamani yake na kuihubiri. Kwa njia nyingine, mafundisho mengi sasa yanadai au kukanusha na kukataa kwamba "*tulinunuliwa* kwa gharama, hata damu ya thamani ya Kristo"na wanaingiza nadharia ya Mageuzi, wakidai kwamba thamani ya Kristo kwa mwenye dhambi inapatikana kwa maneno na mifano yake tu.

Kwa hiyo jua ya Injili kila siku inazidi kusitirika; na japo ukanusho huu wa thamani ya damu kama gharama ya ukombozi wetu haujaendelea toka kwa madhabahu hadi kwa watu, hata hivyo mafundisho ambayo yameshikiliwa kama matakatifu, pamoja na heshima kwa viongozi na mafunzo,yametengeneza njia rahisi kiasi kwamba watu wengi ambao wanaanza kufahamu ili wazingatie mada vile inavyoendelea wamekuwa mateka kwa fundisho la Mageuzi,ambalo

linakana fundisho la Kimaandiko la kuanguka kwa wanadamu na fidia kwake mwanadamu. Maandiko mara nyingi yanatuonya dhidi ya uasi mkubwa, pamoja na kupunguka kwa imani kwa Kanisa kwa wakati huu,ili kwamba Mwana wa Adamu anapokuja apate kama amani imedidimia sana duniani.(*Luka 18:8*). Kitabu cha Zaburi kinaeleza kipindi hiki kwa kusema: "Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam,kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo haitakukaribia wewe [watakatifu waaminifu,washiriki wa mwili wa Kristo, ambao washirika wake walioteuliwa watakamilishwa hivi karibuni]." *Zaburi 91:7.*

Wakati jua la fidia inasitirika, na hata mbalamwezi wa Sheria za Musa, sadaka zake zilizoonyesha fidia, lazima pia zisitirike. Sio hali isio ya kawaida tena kwa walimu wa umma kurejelea dhabihu za damu zilizotolewa na Israeli, ambazo zilihitajika kwa Sheria zao, kama ni ushenzi. Walipoona mwanga wa ukweli wa Neno la Mungu, walikubali maelezo ya Mtume kwamba dhabihu za Israeli zilikuwa ni onyesho ya "dhabihu bora" ya dhambi, lakini sasa, wakikataa mfano, ya fidia,na wakikana dhambi za awali,na mahitaji yake yote ya kuzitoa dhabihu hizo-dhabihu basi ya ukweli pia inakanwa na kudhaniwa kuwa ushenzi, Kwa hiyo kupotea kwa mwanga wa jua ya Injili inasitiri hata mwanga wa mbalamwezi. "Jua litakuwa kama damu." Na *Yoeli (2:10*) inaongeza "nyota huacha kuangaza," ambayo inamaanisha kwamba wakati mwanga wa Injili itasitirika, na Sheria pia zionekane kama hafla za damu zinazokosa maana na za ushenzi, basi mafundisho ya Mungu-nyota kumi na mbili za Kanisa (mitume) pia watapotea kwa mandhari-yaani hazitatambulika kama miongozo ya nuru.

Kama vile tulivyoona, Mungu amechagua nyota kumi na mbili za kitume kwa Kanisa. Kwa hizi na jua na mwezi mwanga wote wa Kanisa ungeendelea.Na kutoka kwa hizi mwanga wa kweli,ambao umebariki Kanisa la kweli,umepata kuendelea.Lakini,Papa,akitaka kuwa bwana wa kanisa la ulimwengu,ameweka ama "kuteua" nyota nyingi,mianga, "mamlaka," "wanathiolojia," katika mwanga wake;na madhehebu mengi ya Kiprotestani pia wamefanya hivyo,hadi idadi imekuwa kubwa mno.Lakini Mungu,akitoa usaidizi,wainjilisti na walimu kwa Kanisa lake la kweli hajawateua kwa mamlaka ya *mwanga* au *nyota*.Badala yake,waumini wake wote wameagizwa kukubali kama miale ya ukweli ambayo yaonekana kutoka kwa jua na mwezi na nyota kumi na mbili *zilizoteuliwa kwa kusudi hilo*.

Watu wa Mungu wengine ambao wanapatikana katika kipindi hiki wanapaswa kuwa na taa iwakayo na kuangaza,hawapaswi kuweka taa zao chini ya kiango,lakini waangaze ili kumtukuza Baba wa mbinguni. Neno nyota (Kiyunani *aster*) halijatumika kurejelea waaminifu (nje na mitume) katika kuwarejelea katika maisha haya;lakini linatumika kurejelea wale ambao wameacha ukweli,na kuwa walimu wa uongo "wanaojivunia" wakitamani kuwa na mamlaka kama mitume,ambao wamekuwa "nyota zipoteazo," "mitume wa uongo." *2 Wakorintho 11:13;Ufu.2:2;Yuda 13*.

Kwa upande mwingine,Maandiko kila mahali yaonyesha ahadi kwamba waaminifu,wanyenyekevu wanaong'aa katika wakati huu watakuwa wazao wa Ibrahimu na Kristo watakaotukuzwa na kuheshimiwa-"nyota ya mbinguni." Lakini siyo katika mbingu za sasa ambazo zitatoweka lakini kwa "mbingu mpya"-ufalme mpya wa miaka elfu.Kwa watu hawa na wakati huo wa ufufuo,Nabii *Danieli (12:3*) anasema, " Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga;na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na

milele.” Mtume Paulo pia ananena kuhusu utukufu wa Kanisa la usoni wakati wa ufufuo,akisema kwamba utukufu wao utakuwa tofauti “iko tofauti ya fahari hata kati ya nyota na nyota.”

Basi ikiwa Mungu aliteua nyota kumi na mbili kama mianga ya Kanisa lake,kama ilivyoonyeshwa katika *Ufunuo (12:1)*,Je! Ni kosa kubwa kwa papa na maaskofu kujiweka kama waandamizi wa mitume-kama nyota pia? Na Je! Siyo hakika kwamba wale wanaoitwa “wakosoaji wakuu” wanajiona na wanaonekana na wengine kama wanaostahili au wakuu kuliko mitume,kama waangazaji wa nuru,nyota? Na wanaonyesha pamoja na wengine wakihubiri dhana zao,wakiangaza nuru zao wenyewe katika mada tofauti,bila kuangalia kwamba inafaa watoe uthibitisho wa maneno yaliyotiwa msukumo na mitume? Na hata wakitaja ama kurejelea toka mafundisho ya mwanga wa nyota za kweli,yaani mitume kumi na wawili,je,si ni kuthibitisha mitazamo na mwanga wao,kuliko kuonyesha kwamba mafundisho kama mwanga kutoka kwa nyota za kitume? Na kwa kweli mwanga wa nyota hizi za uongo, “nyota zipoteazo,” wanapinga sana mwanga kumi mbili uliotiwa msukumo,kiasi cha kwamba wanaweza kupata andiko kutoka kwa maandishi yao.

Katika unabii wa Bwana wetu hii mianga ya kweli ya nyota zinazingatiwa kama sehemu ya Mwanga wa jua ya Injili,ambayo imezimwa,ukatiwa giza;ilhali nyota za uongo,wenye hekima ya kiulimwengu,mianga iliyoteuliwa na wanadamu wa mbingu za sasa zinaonyeshwa zikitoa onyesho kubwa katika hali ya kiulimwemgu-wakiacha kwa kiasi utukufu wa kiroho waliokuwa nao,na kwa mafundisho yao wakaja kwa kiwango cha waadili na wanafilosofia wa kidunia-kwa kiwango cha Wakristo-wananchi-wanasiasa.

Kutikisika kwa mbingu zinazoashiria kanisa lililotajwa kwa uhusiano wa mianga ya Ukristo umeshuka kwa kiwango cha ufunzaji wa umma.Kutikisika huku kungeonyesha kile tunachokiona pande zote-kutikisika kwa Imani na kanuni za Ukristo,ambapo kwa sababu ya mchanganyiko wa makosa,zimeleta machafuko wakati unatajwa kama vile mafundisho ya watoto waliochaguliwa na wasiochaguliwa;mafundisho ya mateso ya milele kwa wale ambao sio watakatifu,na wasioshinda n.k.

Kwa matokeo,wenye hekima wengi wa kiulimwengu wanaotazama hadhara wanajaribu kufanya bidii kuzuia mada zote.Mada gani wanaweza kupata pasi na fundisho la kweli au uwongo wa kuchaguliwa; na dhana ya kweli au uongo wa kutolewa kwa maisha ya baadaye kwa wanadamu? Bila kujua ukweli wa mpango mtakatifu wa awamu,na kukosa kujua utata wa jehanamu na hukumu ya watoto,hawa wahubiri waliobobea wanaweza kuhubiri nini ambacho kitavuta ulimwengu?

Wanaweza kuacha mada zote na kupaa kwa kiwango cha mwanadamu wa kawaida,kwa maswala ua uadilifu na siasa.Wanaweza kuenda kuhubiri injili ya kupinga maisha duni.Wanaweza kuungana katika Mikutano ya Ukristo na uraia,n.k.Na vitu hivi vitashirikisha sana wataalamu wa mimbari;wakati watu wengine wataunda mhemko kwa kupita hata wakafiri wanaosherehekewa katika maelezo ya yale ambayo hawaamini;kwa kutoa rekodi ya Biblia kuhusu maanguko ya Adamu kwa dhambi,na dhana ya kuokolewa kwa kitu ambacho ni Imani potofu,kulingana na nadharia yao ya Mageuzi.

Nani hawezi kuona ishara hizi zikitimilika kwa upande zote leo hii! Lakini jua na mwezi na nyota kumi na mbili kwa sehemu hazieleweki bado;walakini nyota za uongo wengi wameanguka kutoka kwa unafiki wa Injili inayong'aa kwa kiwango cha kufahamu kwa umati wanaowaangaza.

Kwa ajabu,*Luka (21:25,26)* inaongeza ishara za siku: " Tena,kutakuwa na ishara katika jua,na mwezi na nyota;na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukomsuko wake;watu wakivunjika mioyo kwa hofu,na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu.Kwa kuwa nguvu za mbinguni zitatikisika."

Mawimbi yangurumayo ya bahari yanaonyesha kwa ishara umati wa watu wanaohangaika,wamekabiliwa,lakini hawajazuiliwa na sheria na kanuni za jamii.Kila mtu ameisha sikia "msukosuko" kwa miaka ipatayo ishirini iliyopita,na ngurumo za mara kwa mara zinazotokeza kama mawimbi dhidi ya mpango wa kijamii na inataka kuimeza.Zimezuiliwa kwa muda,mawimbi haya yanakusanyika kwa nguvu;na vile yameonyeshwa katika unabii,imebakia miaka michache ili milima (falme) "ziondolewe mpaka katikati ya bahari," katika vurugu.(Zaburi 46:1,2).Kila gazeti,lisilokuwa chini ya mali,sauti zingurumapo za darasa la "bahari";na wengine,japo si kwa kutarajia,lazima itoe mwangwi wa ngurumo za habari.Hii ina maana kwamba wakati wanasema kuna amani basi kutatokea ''shida ya mataifa walio na vurugu."

Na wakati watu wanaanza kugundua kwamba ngurumo za bahari na vurugu zimekuwa hasa imani potofu na ushawishi kwa kikanisa,na wakiendelea zaidi kuona nguvu za mbingu (kanuni za dini za kawaida na mifumo) zikitikisika,basi mioyo yao inawashida kwa hofu-katika wasiwasi wa mambo ambayo yanawajia duniani (jamii);jitihada ya nguvu ambayo inafanyika kusimamisha na kuweka pamoja nguvu za umma na ushawishi,kwa kipimo itafaulu kwa muda mchache;kwa sababu zitasambaratika kabisa.